**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA**

06 Oktoba, 2020

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI KUJITOLEA.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega anawatangazia nafasi za kazi za kujitolea katika jamii karibu na vituo vya kutolea huduma za Afya Vilivyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Busega.

1. **Wakiri Tiba (Lay Counsellors) – Nafasi 20**

**SIFA ZA MWOMBAJI.**

1. Awe na uwezo wa kutunza siri na kuheshimu wateja
2. Awe na uwezo wa kujitolea kusaidia watu / wateja wengine wanaohitaji huduma
3. Awe anajua kusoma na kuandika kwa Kiswahili.
4. Asiwe na tabia ya kuwa nyanyapaa wateja wa CTC na makundi hatarishi katika maambukizi ya VVU.
5. Awe na uwezo wa kutoa elimu ya Afya juu ya UKIMWI kwa mtu mmoja na katika makundi.
6. Awe na uwezo wa kuelewa maswali na kutoa majibu sahihi ya UKIMWI.
7. Awe na uwezo wa kubaini maeneo yenye ushamiri mkubwa wa UKIMWI.

**Vigezo na Masharti ya Waombaji:**

1. Awe Raia wa Tanzania
2. Awe ni mteja mwenye ufuasi mzuri wa dawa.
3. Awe anaishi katika eneo analoomba kufanyia kazi
4. Awe na umri usiozidi miaka 45 na usiopungua miaka 18
5. Atafanya kazi katika jamii anayo ishi na katika kituo kinacho hudumia jamii hiyo.

**NB: Awe amefanya kazi hii na mashirika mengine katika Halmashauri ya Busega**

Barua zote ziwasilishwe kwa Mganga Mfawidhi katika kituo cha kutolea huduma ambacho kipo karibu na makazi yako.

Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 21 Octoba 2020. Nafasi hizi ni za muda wa mwaka mmoja na zinahuishwa baada ya muda kuisha kutegemeana na uwajibikaji wako.

Limetolewa na

Anderson Njiginya Kabuko
Mkurugenzi Mtendaji (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA.

MKURUGENZI MTENDAJI
'H/ WILAYA YA BUSEGA'

Sanduku la Posta 157, Busega; Simiyu; simu-+255 (028) 2981193, Nukushi- +255 (028)2981194
Barua pepe: ded@busegadc.go.tz na Tovuti: www.busegadc.go.tz

Scanned with CamScanner

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA

06 Oktoba, 2020

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega anawatangazia nafasi za ajira kwa mkataba wa mwaka mmoja katika vituo vya kutolea huduma na tiba. Hivyo basi Watanzania wote wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi za kazi zilizoainishwa hapo chini watume maombi.

**2. WASAIDIZI WA HESABU (nafasi 4) TGS B1**

**a) Sifa za kuajiriwa**

Waajiriwa wenye cheti cha **ATEC Level II au "Foundation Level"** kinachotolewa na NBAA, waombaji wawe na uzoefu wa kazi Zaidi ya Mwaka (1) katika fani hiyo.

**b) Kazi na majukumu**

i. Kuandika na kutunza "Register" zinazohusu shughuli za uhasibu
ii. Kuandika hati za malipo na hati za mapokezi ya fedha
iii. Kutunza majalada yenye kumbukumbu za hesabu
iv. Kupeleka barua / nyaraka za uhasibu Benki
v. Kufanya usuluhisho wa masurufu, karadha, hesabu za Benki na Amana.

**MASHARTI YA UJUMLA KWA WAOMBAJI**

1. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45
2. Waombaji wote waambatishe nakala ya cheti cha kuzaliwa
3. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo binafsi CV, nakala za vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waloifika kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.

Sanduku la Posta 157, Busega; Simiyu; simu-+255 (028) 2981193, Nukushi- +255 (028)2981194
Barua pepe: ded@busegadc.go.tz na Tovuti: www.busegadc.go.tz

Scanned with CamScanner

4. Picha moja passport Size iandikwe jina kwa nyuma
5. Hati za matokeo ya kidato cha nne na sita (Statement of Result havitakubalika)
6. Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya Kingereza au Kiswahili na yatumwe kwa njia ya Posta kabla ya tarehe ***21/10/2020*** kwa anwani ifuatayo.

Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya
S.L.P 157,
**BUSEGA.**

Anderson N. Kabuko
Mkurugenzi Mtendaji
**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA.**

MKURUGENZI MTENDAJI
H/ WILAYA YA BUSEGA



Scanned with CamScanner

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA**

06 Oktoba, 2020

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega anawatangazia nafasi za kazi watu wote wenye Taaluma na ambao wako tayari kufanya kazi katika vituo vya kutolea huduma za Afya vilivyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Busega.

## 1. AFISA TABIBU (Nafasi 1)

### SIFA ZA KUAJIRI

Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne/sita wenye Stashahada ya Tabibu kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali.

**Kazi na majukumu:**

(i) Kutambua na kutibu wagonjwa katika vituo vya huduma na tiba na mafunzo ya UKIMWI (CTC)

(ii) Kusimamia huduma za upimaji katika vituo vya tiba na matunzo ya UKIMWI (CTC)

(iii) Kushiriki katika kupanga na kutekeleza Huduma za Afya Msingi

(iv) Kushauri na kuhamasisha wananchi kupima maambukizi ya UKIMWI katika vituo vya tiba na matunzo UKIMWI

(v) Kuweka kumbukumbu za vifaa na zana za kutolea huduma

(vi) Kuweka kumbukumbu, kuandaa na kutoa taarifa za utekelezaji katika vituo vya tiba na matunzo (CTC)

## MUUGUZI DARAJA LA II –(Nafasi 2)

### a) Sifa za kuajiriwa

Kuajiriwa wenye cheti cha Uuguzi cha miaka miwili kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali na kuandikishwa (Enrolled) na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania.

Sanduku la Posta 157, Busega; Simiyu; simu-+255 (028) 2981193, Nukushi- +255 (028)2981194
Barua pepe: ded@busegadc.go.tz na Tovuti: www.busegadc.go.tz

Scanned with CamScanner

**b) Kazi na Majukumu**

(i) Kufanya kazi za kiuguzi za kuhudumia wateja katika jamii,katika vituo vya tiba na matunzo ya UKIMWI.

(ii) Kusimamia na kuratibu kazi zote za wahudumu wa afya katika vituo vya tiba na matunzo ya UKIMWI

(iii) Kukusanya takwimu na kutayarisha taarifa za utendaji wake wa kazi katika vituo vya huduma na matunzo ya UKIMWI

(iv) Kutoa huduma kwa wagonjwa majumbani.

(v) Kutoa ushauri nasaha kupima katika vituo vya huduma na matunzo ya UKIMWI

(viii) Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu maambukizi ya UKIMWI

**VIGEZO NA MASHARTI YA WAOMBAJI**

I. Awe raia wa Tanzania
II. Awe na umri usiozidi miaka 45 na usiopungua miaka 18
III. Maombi yote yaambatanishwe na nakala ya Cheti cha Taaluma, nakala ya Cheti cha kidato cha nne/sita, Maelezo binafsi (CV), Picha (Passporti mbili ) za hivi karibuni.
IV. Vyeti vyote vya taaluma na kidato cha nne/sita lazima vithibitishwe na Hakimu au wakili anayetambulika na Serikali.
V. Mwombaji yeyote ambaye hatazingatia mojawapo ya masharti au vigezo tajwa hapo juu, maombi yake hatashughulikiwa.

**1. DATA CLERK (Nafasi 2)**

**a) Sifa za kuajiriwa**

I. Kuajiriwa Awe na Cheti katika fani zifuatazo:-

- Utunzaji kumbukumbu za Kiafya (Health Record and Information Management), Information Technology (IT)., Takwimu, Computer (Health Data Experience) awe na uzoefu wa kutumia Mfumo wa DHIS, ***EXCEL, MS, ACCESS, PEINFO, SSP*** na uzoefu wa mifumo mingine itakuwa sifa ya ziada.



Scanned with CamScanner

b) **Kazi na Majukumu**

i. Utunzaji wa Mfumo wa CTC, Data Base

ii. Kuhuisha CTC Data Base

iii. Kuingiza Takwimu za Wagonjwa kila siku na kutengeneza taarifa na kuwasilisha katika ngazi husika

iv. Kurudisha faili za wagonjwa ambao hazijajazwa kwa Mganga (Clinical Zirekebishwe)

v. Kuhakikisha kila file la Mgonjwa linakuwa na fomu ya kuchunguza ugonjwa wa kifua kikuu na magonjwa ya STI na kuhakikisha zinajazwa na Mganga kila Mgonjwa anapohudhuria Kliniki.

vi. Kutengeneza mpango kazi wa kuboresha takwimu katika kituo husika katika Mfumo wa CTC, Data Base na ktika vyanzo vya Takwimu

vii. Kuhakikisha matumizi sahihi ya mfumo unafanya kazi kila siku, kila wakati kuhusisha nati virus kila siku

viii. Kuhakikisha unawasiliana na viongozi wako kwa wakati kwa ajili ya kukarabati Mfumo pindi tatizo linapotokea

ix. Kuingiza Data CTC 2 waishio na VVU/ Ukimwi kwenye Komputa

x. Kusafisha Data husika kila mara katika Data ya Mradi

xi. Kuandaa ripoti za kila mwezi na kuwasilisha kwa msimamizi wake wa kazi pamojana majukumu mengine atakayopangiwa na mwajiri.



Scanned with CamScanner

**MUDA WA MKATABA: MIEZI KUMI NA MBILI (12)**
Mishahara italipwa kwa ufadhili wa shirika la Amref Tanzania katika kutekeleza Mradi wa Afya kamilifu.

Barua zote zitumwe kwa njia ya posta, maombi yatakayowasilishwa kwa njia ya mkono au barua pepe hayatafanyiwa kazi.

Mwisho wa kupikea barua za maombi ni tarehe 21 Oktoba, 2020

Barua zitumwe kwa njia ya posta kupitia anuani ifuatayo
Mkurugenzi Mtendaji (W)
S.L.P 157,
**BUSEGA.**

Limetolewa na

Anderson Njiginya Kabuko
Mkurugenzi Mtendaji
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA

MKURUGENZI MTENDAJI
H/ WILAYA YA BUSEGA

Sanduku la Posta 157, Busega; Simiyu; simu-+255 (028) 2981193, Nukushi- +255 (028)2981194
Barua pepe: ded@busegadc.go.tz na Tovuti: www.busegadc.go.tz

Scanned with CamScanner